JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

# 03 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................... iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI ........................................................................ 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha ........................ 2

2.1.1 Swali la 1: Kufuata Kanuni Za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali. ........................................................ 3

2.1.2 Swali la 2: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka................................................... 12

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi ...................................... 18

2.2.1 Swali la 3: Kutambua Msingi ya Uzalendo katika Jamii. ...... 19

2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku ........................................................ 29

3.0 TATHMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI.......................... 35

4.0 HITIMISHO ........................................................................ 35

5.0 MAPENDEKEZO .................................................................. 36

KIAMBATISHO........................................................................ 37

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2020 kwa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa, stadi na mielekeo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza au kutojifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri kwani asilimia 94.81 walifaulu.

Katika taarifa hii, sababu zilizochangia ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika somo la Maarifa ya Jamii zimeainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali umetokana na uelewa mzuri wa mahitaji ya kila swali na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Pamoja na hayo, wanafunzi ambao hawakufaulu vizuri ni wale ambao walishindwa kutambua matakwa ya maswali kutokana na umahiri mdogo katika stadi za kusoma na kuandika. Wanafunzi wengine hawakuwa na umahiri wa kutosha katika maeneo yaliyotahiniwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri ulifanyika na kuonesha kuwa, katika kila umahiri uliopimwa, wanafunzi wamefanya vizuri. Hata hivyo, jitihada zaidi katika ufundishaji wa somo la Maarifa ya Jamii zinatakiwa kuwekwa katika umahiri mkuu unaohusu Matumizi ya Ramani na Elimu ya Anga katika maisha ya kila siku. Umahiri huu ulionekana kuwa na ufaulu wa chini ikilinganishwa na umahiri mwingine katika somo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa mrejesho unaotokana na ripoti hii utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia, Baraza linatarajia kuwa mamlaka husika zitahakikisha dosari zilizoainishwa katika

taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza umahiri kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuingia darasa la tano.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA 2020) ulifanyika tarehe 25 na 26 Novemba 2020. Jumla ya watahiniwa 1,828,268 (100%) walisajiliwa kufanya upimaji katika somo la Maarifa ya Jamii, ambapo watahiniwa 1,702,385 (93.11%) walifanya upimaji. Watahiniwa 1,614,207 sawa na asilimia 94.81% walifaulu.

Karatasi ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali 25. Maswali haya yaligawanywa katika sehemu kuu mbili: A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 2 ambayo ni swali la 1 na la 2 yenye jumla ya vipengele 14 kutoka katika mahiri kuu mbili. Mahiri hizo ni *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* (swali la 1(i) hadi (viii), *na Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* (swali la 2(i) hadi (vi). Aidha, sehemu B ilikuwa na maswali 2, ambayo ni swali la 3 na la 4 yenye jumla ya vipengele 11 kutoka katika mahiri kuu mbili. Mahiri hizo ni *Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* (swali la 3(i) hadi (vii), na *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* (swali la 4(i) hadi (iv). Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili. Aidha, sehemu A ilikuwa na swali la 1 na la 2 ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuoanisha maelezo ya fungu A na yale ya fungu B. Kisha walitakiwa kuandika herufi kwenye mabano. Sehemu B ilikuwa na swali la 3, ambalo wanafunzi walitakiwa kusoma habari (majadiliano), na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Swali la 4 (i) hadi (iv) liliwataka wanafunzi kuchunguza na kuandika vitu vinavyowakilishwa na alama za ramani.

Katika taarifa hii, utangulizi utafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi unabainisha umahiri wa

wanafunzi, ukiambatana na majibu yao ambayo ama yalikuwa ya kiwango kizuri, cha wastani, au dhaifu kulingana na swali husika. Sababu za kila kundi kuwa na umahiri waliouonesha pia zitachambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali utafuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo itafuatiwa na hitimisho na baadaye mapendekezo yatakayotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vilizingatia asilimia ya wanafunzi waliofanya swali husika. Iwapo watahiniwa kati ya asilimia 0 hadi 33 tu ndio walioweza kujibu swali hilo vizuri, kiwango hiki cha ufaulu kilihesabika kuwa ni **hafifu**. Kwa upande mwingine, kama wanafunzi walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 34 hadi 66, ufaulu huo ulihesabika kuwa ni wa ***wastani,*** na kiwango cha ufaulu kilihesabika kuwa ni ***kizuri*** iwapo watahiniwa walioweza kufanya swali hilo vizuri ni kati ya asilimia 67 hadi 100. Katika uchambuzi huu, rangi za kijani, njano na nyekundu zinatumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu, mtawalia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kilikuwa kizuri katika swali la kwanza na la pili na cha wastani katika swali la tatu na nne. Katika sehemu hii, kila swali limechambuliwa na utendaji wa wanafunzi kubainishwa. Vielelezo vimetumika kuthibitisha hoja zilizotolewa katika kila swali.

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye jumla ya vipengele 14. Swali la kwanza lilikuwa na vipengele nane vya maswali ya kuchagua, ambapo mwanafunzi alitakiwa kusoma

swali na kisha kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo aliyopewa. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha, ambalo lilikuwa na vipengele sita: kila mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka Fungu A na kuoanisha na jibu sahihi kutoka Fungu B.

### 2.1.1 Swali la 1: Kufuata Kanuni Za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali

Swali hili lilikuwa na vipengele nane, vilivyopima umahiri wa *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali.* Wanafunzi walitakiwa kusoma vipengele, kuchagua herufi ya jibu sahihi, na kuandika katika kisanduku kilichoachwa wazi. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16.


Katika swali hili, mwanafunzi alihesabika kuwa na utendaji hafifu iwapo alishindwa kujibu kipengele hata kimojawapo, au aliweza kujibu vipengele viwili peke yake. Mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa ufasaha vipengele vitatu hadi vitano alikuwa na utendaji wa wastani, na mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele sita hadi saba alikuwa na utendaji mzuri. Kwa upande mwingine, mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote vinane alikuwa na utendaji mzuri *sana*.

Jumla ya wanafunzi 1,702,385 (100%) walijibu swali hili. Miongoni mwao, wanafunzi 59,501 (3.50%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi 247,189 (14,52%) walikuwa na utendaji mzuri: waliweza kujibu kwa usahihi vipengele kati ya sita na saba vya swali hilo.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 857,333 (50.36%) walikuwa na utendaji wa wastani. Kati yao, wanafunzi 340,424

(20.00%) walipata kwa usahihi vipengele vitatu; 296,754 (17.43%) walipata vipengele vinne; na 220,096 (12.93%) walipata vipengele vitano.

Aidha, wanafunzi 538,362 (31.62%) walikuwa na utendaji hafifu, hivyo kutofaulu swali hilo. Kati yao, 55,343 (3.25%) hawakuweza kujibu kwa usahihi kipengele chochote cha swali hilo. Wengine 182,532 (10.72%) waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu, wakati 300,487 (17.65%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele viwili. **Chati Na. 1** inaonesha mchanganuo wa viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




***Chati Na 1:*** *Umahiri wa wanafunzi katika kila kundi ambapo ufaulu wa jumla ni mzuri*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika na kubaini mambo mbalimbali yanavyooneshwa katika kila swali kama ifuatavyo:

(i) Kwa nini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?

A Kinapendwa na watu wengi

B Kinavutia watalii wengi

C Kinaajiri watu wengi

D Kinavutia uchimbaji wa madini

Kipengele hiki kilipima umahiri wa *Kutambua Shughuli za Uzalishaji Mali katika Jamii.* Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua sababu inayofanya kilimo kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi *C, Kinaajiri watu wengi,* walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mchango wa kilimo katika kukuza uchumi wa Tanzania.

Hata hivyo, wapo waliochagua kipotoshi *A*, *Kinapendwa na watu wengi*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha kuwa wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa kilimo si shughuli rahisi hapa Tanzania na watu wanaofanya kazi hii hutumia nguvu nyingi na hukabiliana na changamoto nyingi. Zaidi ya yote, watu wengi, hasa vijana, hawapendi kilimo. Hivyo, hukimbilia mijini kwa ajili ya kupata kazi au shughuli nyingine inayoingiza kipato tofauti na kilimo. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Kinavutia watalii wengi* walishindwa kutambua kuwa vivutio vya utalii ni pamoja na mbuga za wanyama, milima, maeneo ya kihistoria na fukwe. Kilimo si miongoni mwa vivutio vya utalii. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kinavutia uchimbaji wa madini,* walishindwa kuelewa kuwa shughuli ya uchimbaji wa madini huvutiwa na sera nzuri za nchi, upatikanaji wa madini, mitaji na masoko ya madini

husika. Kwa upande mwingine, uchimbaji wa madini huathiri shughuli za kilimo kwa kupunguza eneo linaloweza kutumika kwa kilimo na kusababisha madhara kama mmongonyoko wa udongo.

(ii) Nchi ya Tanzania inafaidika vipi na uchimbaji wa madini?

A Kupata fedha za kigeni

B Kuongezeka kwa mazao

C Kuongezeka kwa mifugo

D Kuongezeka kwa misitu

Kipengele cha swali hili kilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Shughuli za Uzalishaji Mali katika Jamii*. Kilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini faida za uchimbaji wa madini nchini Tanzania. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili kwa kuchagua jibu sahihi *A, Kupata fedha za kigeni,* walikuwa mahiri kuhusu umuhimu wa biashara ya madini inchini Tanzania kwani madini ni mali na yana thamani kubwa sana. Kutokana na madini kuwa na thamani, soko la bidhaa hiyo limekuwa likivutia wateja wengi kutoka ndani na nje ya nchi. Hivyo, huwezesha kupatikana kwa fedha za kigeni.

Wanafunzi waliochagua vipotoshi B, *Kuongezeka kwa mazao*; *C, Kuongezeka kwa mifugo*; *na D, Kuongezeka kwa misitu*, walielewa kuwa kuongezeka mazao na mifugo ni faida ya uchimbaji wa madini, jambo ambalo si sahihi. Uchimbaji wa madini husababisha kukosekana kwa eneo la kilimo na kulisha mifugo. Pia hupunguza misitu kupitia kusafisha eneo kwaajili ya uchimbaji. Hivyo vipotoshi hivi vyote si faida ya uchimbaji wa madini.

(iii) Ni athari ipi ya uharibifu wa mazingira **haisababishwi** na uchimbaji wa madini?

A Ukataji wa miti ovyo

B Ongezeko la mvua

C Uchafuzi wa maji

D Kuwepo mashimo makubwa

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi*. Kilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini athari ya uharibifu wa mazingira isizosababishwa na uchimbaji wa madini. Kwa mwanafunzi kujibu kipengele hiki kwa usahihi alipaswa kuwa na umahiri wa kubainisha athari zote katika vipotoshi zinazosababishwa na uchimbaji wa madini, ambazo ni A, *Ukataji wa miti*; C, *Uchafuzi wa maji*; na D, *Kuwepo mashimo makubwa*. Hivyo, wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi B, *Ongezeko la Mvua* walikuwa na uelewa wa kutosha kwamba mvua haiongezeki kutokana na uchimbaji wa madini, isipokuwa kuongezeka kwa uvukizaji kutoka kwenye vyanzo vya maji na mimea.

Baadhi ya wanafunzi walishindwa kuchagua jibu sahihi. Hivyo, walichagua vipotoshi *A, Ukataji wa miti ovyo; C, Uchafuzi wa maji;* na *D, Kuwepo kwa mashimo*. Wanafunzi hawa hawakuwa na umahiri wa kutosha kwa kuwa uchimbaji wa madini husababisha ukataji wa miti ili kupata eneo la kuchimba. Aidha, uchimbaji wa madini huzalisha vumbi ambalo husababisha uchafuzi wa hewa. Pia, madini huitaji kusafishwa kwa kutumia kemikali na maji; hivyo, uathiri vyanzo vya maji. Kwa upande mwingine, uwepo wa mashimo ni matokeo ya uchimbaji wa madini. Mashimo haya hufanya

ardhi husika isiwe rafiki kwa shughuli nyingine ya uzalishaji mali, hususani kilimo.

(iv) Ipi ni faida ya mbuga za wanyama nchini Tanzania?

A Kuongeza pato la Taifa

B Kupata samadi ya kilimo

C Kuongezeka kwa wawindaji haramu

D Kupata ardhi nzuri ya kilimo

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi*. Kipengele hiki kililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kutambua faida za mbuga za wanyama nchini Tanzania. Umahiri wa wanafunzi katika kujibu swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Kuongeza pato la Taifa*.

Pamoja na ufaulu huo, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kupata samadi ya kilimo,* walishindwa kubaini kuwa wanyamapori hawazalishi samadi kama ilivyo kwa wanyama wafugwao ambao huzalisha samadi inayotumika kurutubisha udongo kwa ajili ya kilimo. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Kuongezeka kwa wawindaji haramu*, walishindwa kubaini kuwa uwindaji haramu husababisha kuuwawa kwa wanyamapori. Hivyo, husababisha hasara kwa taifa. Kwa upande wa wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Kupata ardhi nzuri ya kilimo*, walishindwa kubaini kuwa mbuga za wanyama hazitumiki kwa ajili ya shughuli zingine za uzalishaji mali zaidi ya utalii na uhifadhi.

(v) Ni kwa nini matumizi ya baruti na sumu hayakubaliki katika shughuli za uvuvi?

A Huua samaki wengi kwa wakati mmoja

B Huwapa wavuvi hasara kubwa

C Hunasa samaki wakubwa tu

D Husababisha wavuvi kukosa ajira

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi*. Kilipima umahiri wa mwanafunzi katika kutambua athari itokanayo na matumizi ya baruti na sumu, ambazo ni njia za uvuvi haramu. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *A, Huua samaki wengi kwa wakati mmoja,* walikuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha kutambua zana mbalimbali za uvuvi na athari zake.

Aidha, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *B, Huwapa wavuvi hasara kubwa,* walihusianisha neno kuua na hasara, jambo ambalo si sahihi kwani njia hizi haramu huwawezesha wavuvi kupata samaki wengi; samaki huvuliwa hata wakiwa wamekufa. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *C, Hunasa samaki wakubwa tu*. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutambua kuwa sumu na baruti hazichagui samaki wa kuua. Hivyo, huua samaki wa aina na ukubwa wowote. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Husababisha wavuvi kukosa ajira,* walikosa umahiri wa kutambua kuwa zana hizi huwezesha upatikanaji wa samaki wengi. Hivyo, huitaji watenda kazi wengi.

(vi) Ni madini yapi yanapatikana nchini Tanzania tu?

A Tanzanaiti

B Dhahabu

C Almasi

D Chokaa

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutambua Shughuli za Uzalishaji Mali katika Jamii*. Kilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini aina ya madini yanayopatikana Tanzania tu. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *A, Tanzanaiti*, walikuwa na umahiri wa kutosha kutambua aina mbalimbali za madini yanayopatikana Tanzania. Pia, jina la madini hayo "Tanzanaiti" lina shabihiana kwa kiasi kikubwa na jina la nchi. Hivyo, wanafunzi waliweza kuhusisha jina la nchi na jina la madini hayo.

Aidha, baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Dhahabu*. Uchaguzi huu unatokana na umaarufu wa madini haya hapa nchini. Pia, maeneo maarufu kama Bulyanhulu na Buzwagi pamoja na makampuni makubwa kama Barrick na Geita Gold Mine yamepelekea wanafunzi kufikiri kuwa dhahabu hupatikana Tanzania tu. Wapo wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Almasi.* Wanafunzi hawa hawajui kuwa Almasi inapatikana maeneo mbalimbali duniani, tofauti na Tanzanaiti inayopatikana Tanzania pekee. Kipotoshi *D, Chokaa,* kilichaguliwa na wanafunzi waliokosa maarifa kuhusu madini mbalimbali na maeneo yanapopatikana.

(vii) Nini kifanyike ili kurekebisha eneo lililoathiriwa na shughuli za uchimbaji wa madini?

A Kufuga mifugo mingi

B Kusafisha ardhi

C Kumwagilia maji

D Kupanda miti

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa Kuthamini na Kulinda Rasilimali za Nchi. Kililenga kupima umahiri wa wanafunzi kubaini njia sahihi ya kutunza mazingira yaliyoharibiwa na shughuli za uchimbaji madini. Wanafunzi wengi walioweza kuchagua jibu sahihi *D, Kupanda miti*, walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu njia bora ya kurekebisha madhara yatokanayo na shughuli za uchimbaji wa madini.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Kufuga mifugo mingi,* walishindwa kubaini kuwa kitendo hiki husababisha uharibufu zaidi wa mazingira kwani kwato na ulaji majani hulifanya eneo kuathiriwa na mmomonyoko wa udongo. Wanafunzi wengine waliochagua vipotoshi *B, Kusafisha ardhi* na *C, Kumwagilia maji,* walishindwa kubaini kuwa vitendo hivi huifanya ardhi kumomonyoka kwa urahisi, hivyo kuongeza madhara zaidi.

(viii) Ni fursa ipi ya kiuchumi inayotokana na misitu?

A Uzalishaji wa nafaka

B Shughuli za uvuvi

C Shughuli za urinaji wa asali

D Uchimbaji wa madini

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa Kutambua Shughuli za Uzalishaji Mali Katika Jamii. Kilipima umahiri wa wanafunzi kubaini fursa ya kiuchumi inayotokana na misitu. Wanafunzi walioweza kuchagua jibu sahihi *C, Shughuli za urinaji wa asali*, walikuwa na umahiri wa kutosha kutambua kuwa shughuli ya urinaji wa asali hutokana na nyuki ambao huishi kwenye misitu.


Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi *A, Uzalishaji wa nafaka*. Hawa walikosa umahiri wa kubaini kuwa nafaka hupatikana kutokana na kilimo, ambacho hakifanyiki katika misitu. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Shughuli za uvuvi,* walikosa umahiri wa kubaini kuwa uvuvi hufanyika maeneo yenye maji kama mito, maziwa, na bahari. Wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Uchimbaji wa madini*, walikosa umahiri wa kubaini kuwa uchimbaji wa madini husababisha kupotea kwa misitu, kwani kitendo cha kuchimba ardhi husababisha kutoweka kwa mimea.

### 2.1.2 Swali la 2: Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka

Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kujibu kipengele cha (i) hadi cha (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa Fungu A, na majina ya vifaa husika kutoka Fungu B, walitakiwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu 1: Kutambua *Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka,* hususani kutoka katika umahiri mahususi *1.3: Kutumia Elimu ya Hali ya Hewa Katika Shughuli za Kila Siku.* Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi katika kutambua

vifaa mbalimbali vinavyotumika kupima hali ya hewa. Jumla ya alama kwa swali hili zilikuwa 12.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,385 (100%), ambapo wanafunzi 121,082 (7.11%) walipata alama zote 12, ambao ni ufaulu mzuri sana, na wanafunzi 288,520 (16.95%) walipata alama 8 hadi 10, ambao ni ufaulu mzuri. Hata hivyo, wanafunzi 736,749 (43.28%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 555,957 (32.66%) walipata alama 0 hadi 2 ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ukizingatia kuwa wanafunzi 1,146,428 (67.34%) walipata alama 4 hadi 12 kama **Chati Na. 2** inavyoonesha.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 121,082 (7.11%) walipata alama za juu, ambazo ni kati 10 hadi 12. Hii inaashiria kuwa

wanafunzi hawa walikuwa na uelewa mkubwa na maarifa ya kutosha juu ya umahiri mkuu unaohusu *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka,* hasa umahiri mahsusi unaohusu *Kutumia Elimu ya Hali ya Hewa Katika Shughuli za Kila Siku*. Wanafunzi hawa waliweza kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa na majina ya vifaa husika. **Kielelezo Na. 1.1** kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( D ) | A. Haigromita<br>B. Kampbeli Stok |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( A ) | C. Kipimajoto |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( G ) | D. Kipima upepo<br>E. Kipima mvua |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( C ) | F. Anemomita<br>G. Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( F ) | H. Stevenson screen |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( B ) | |

**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 2*

Hata hivyo, wanafunzi 288,520 (16.95%) walimudu kuoanisha vipengele 5 kati ya 6. Wanafunzi hawa walielewa baadhi ya vifaa na matumizi yake. Baadhi ya wanafunzi walimudu kuoanisha kwa usahihi vipengele (i), (ii), (iii), (iv) na (v) vya Fungu A kwa herufi “D”, “A”, “G”, “C” na “F” kutoka Fungu B. Kwa mfano, katika kipengele cha (iv), wanafunzi walioanisha kwa usahihi kifaa kinachotumika kupima jotoridi kutokana na

umaarufu wa kifaa hiki uliotokana na ugonjwa wa korona. Pia, hutumika zaidi katika hosipitali mbalimbali. Wanafunzi hawa pia walishindwa kuoanisha kipengele (vi) kwa kuwa jina la kifaa hiki si maarufu sana katika mazingira yao ya ufundishaji na ujifunzaji. Jina maarufu au lililozoeleka kwa wanafunzi wengi ni kipima mwanga wa jua. **Kielelezo Na 1.2** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (vi) katika swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( D ) | A. Haigromita<br>B. Kampbeli Stok |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( A ) | C. Kipimajoto |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( G ) | D. Kipima upepo<br>E. Kipima mvua |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( C ) | F. Anemomita<br>G. Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( F ) | H. Stevenson screen |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( E ) | |

**Kielelezo Na. 1.2:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele (vi) cha swali la 2*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa 736,749 (43.28%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata kati ya alama 4 hadi 6. Wanafunzi 316,369 (18.58%) walipata alama 6; hii inaonesha kuwa waliweza kujibu

vipengele 3 kati ya 6 vya swali hili. Wengi wa wanafunzi hawa walijibu kwa usahihi kipengele (i), (iv) na (v). Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawa walikuwa na umahiri wa kutosha juu ya vifaa vinavyotumika kupima uelekeo wa upepo, jotoridi, na mwendo kasi wa upepo. **Kielelezo Na 1.3** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 katika swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( D ) | A. Haigromita<br>B. Kampbeli Stok |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( F ) | C. Kipimajoto |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( B ) | D. Kipima upepo<br>E. Kipima mvua |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( C ) | F. Anemomita<br>G. Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( F ) | H. Stevenson screen |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( A ) | |

**Kielelezo Na. 1.3:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi kipengele (i), (iv) na (v)*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 555,957 (32.66%) walikuwa na ufaulu hafifu. Kati yao, 333,734 (19.60%) walipata alama 2 kwani waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu cha swali hili. Kipengele (iv) ndicho kilijibiwa na wanafunzi wengi zaidi kutokana na ukweli kuwa ni kifaa kinachotumiwa zaidi hasa katika kipindi hiki cha janga la korona. **Kielelezo Na 1.4** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu cha swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| **Fungu A** | **Herufi** | **Fungu B** |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( E ) | A. Haigromita<br>B. Kampbeli Stok |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( F ) | C. Kipimajoto |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( A ) | D. Kipima upepo<br>E. Kipima mvua |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( C ) | F. Anemomita<br>G. Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( G ) | H. Stevenson screen |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( D ) | |

**Kielelezo Na. 1.4:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kipengele (iv) tu*

Aidha, wanafunzi 222,223 (13.05%) walipata alama 0. Hawa hawakuwa na maarifa juu ya umahiri mkuu unaohusu *Kutambua Matukio Yanayotokea Katika Mazingira Yanayomzunguka,* hasa umahiri mahsusi unaohusu *Kutumia Elimu ya Hali ya Hewa Katika Shughuli za Kila Siku*. Wanafunzi hawa walishindwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa na majina ya vifaa hivyo. Hali hii inaashiria kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na umahiri uliotarajiwa katika kupima hali ya hewa. **Kielelezo Na 1.5** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha maelezo ya vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa katika **Fungu A** na majina ya vifaa husika katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| **Fungu A** | **Herufi** | **Fungu B** |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( A ) | A. Haigromita<br>B. Kampbeli Stok |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( E ) | C. Kipimajoto |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( F ) | D. Kipima upepo<br>E. Kipima mvua |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( G ) | F. Anemomita<br>G. Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( A ) | H. Stevenson screen |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( E ) | |

**Kielelezo Na. 1.5:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali la 2*

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi. Katika swali la 3, wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hilo lilikuwa na jumla ya vipengele saba vyenye alama 2 kila kimoja, hivyo kufanya jumla ya alama 14. Katika swali la 4, mwanafunzi alitakiwa kuchunguza alama alizopewa na kisha kuandika majina yanayowakilishwa na alama hizo. Swali hilo lilikuwa na vipengele 4. Kila kipengele kilikuwa na alama 2, hivyo kufanya kuwa na jumla ya alama 8. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu katika maswali yote mawili ulikuwa wa wastani, ingawa ufaulu katika swali la 4 ulikuwa chini ukilinganishwa na ufaulu katika swali la 3. Uchambuzi zaidi kwa kila swali ni kama ifuatavyo.

### 2.2.1 Swali la 3: Kutambua Msingi Ya Uzalendo Katika Jamii.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu *Kutambua Msingi ya Uzalendo katika Jamii* na umahiri mahususi *Kudumisha Utamaduni wa Mtanzania*. Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma habari (majadiliano) kuhusu utamaduni wa kusalimiana (Tazama Kielelezo Na. 1.6) na kisha kujibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi. Swali lilikuwa na vipengele saba, yaani (i) hadi (vii). Kipengele cha (i) kilipima ufahamu wa wanafunzi kutambua kabila la Masatu. Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini mtindo wa kusalimiana anaupenda Dihenga. Kipengele cha (iii) kilipima uwezo wa mwanafunzi kutambua ngoma wanayocheza Wazaramo na kipengele cha (iv) kililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua kabila ambalo watu wake wanasalimiana kwa kushikana mikono. Aidha, kipengele cha (v) kilipima uwezo wa mwanafunzi kutathmini faida ya kucheza ngoma ya mdundiko kutokana na taarifa aliyosoma. Vilevile, kipengele cha (vi) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini namna mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalivyoanza, na kipengele cha (vii) kilipima ufahamu wa wanafunzi kuhusu funzo walilopata kutokana na habari waliyosoma. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 14. **Kielelezo Na. 1.6** kinaonesha habari iliyotumika katika swali la 3.

Soma majadiliano yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

**Dihenga**: Hujambo?
**Masatu:** Sijambo
**Dihenga**: Hivi wewe ni kabila gani?
**Masatu:** Mimi ni Msukuma, wewe je?
**Dihenga**: Mimi ni Mzaramo.
**Masatu:** Nimesikia jana ulikuwa unacheza ngoma katika sherehe.
**Dihenga**: Ndiyo tulikuwa tunacheza ngoma iitwayo mdundiko. Wewe hupendelea ngoma gani?
**Masatu:** Na mimi pia napenda mdundiko kwa sababu mwili unakuwa imara.
**Dihenga**: Je unapendelea kusalimia watu katika jamii yako?
**Masatu:** Ndiyo mara nyingi ninasalimia watu mbalimbali katika jamii yangu.
**Dihenga**: Mnasalimiaje katika jamii yako?
**Masatu:** Tunasalimiana kwa kushikana mikono, wewe je?
**Dihenga**: Mimi napenda kusalimiana kwa kukumbatiana.
**Masatu:** Ooh! Hongera.
**Dihenga:** Ahsante.

**Maswali**

(i) Masatu ni kabila gani? ___________________________________

(ii) Dihenga hupendelea kusalimiaje? ___________________________

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo.______________________

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono?______________________________________


(v) Taja faida moja ya kucheza ngoma ya 'mdundiko'. ______________________________________________________

(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje? _____________________________________________

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo?________________________________________

**Kielelezo Na. 1.6** kinaonesha kifungu cha habari ambacho wanafunzi walitakiwa kusoma na kisha kujibu swali la 3.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,385 (100%), ambapo wanafunzi 141,939 (8.4%) walipata alama zote 14, ambao ni ufaulu mzuri sana. Wanafunzi 258,781 (33.6%) walipata alama kati ya 10 hadi 12, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 242,162 (24.4%) walipata alama kati ya 6 hadi 8, ambao ni ufaulu wa wastani. Pia, wanafunzi 124,952 (33.6%) walipata alama kati ya 0 hadi 4, ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa wanafunzi 1,577,433 (66.4%) walipata kati ya alama 6 hadi 14. **Chati Na. 3** inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 66.4 ya wanafunzi waliweza kupata alama kati ya 6 hadi 14*.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kulikuwa na tofauti kubwa kati ya majibu yaliyotolewa na wanafunzi waliopata alama 10 – 12 (asilimia 33.6) na wale waliopata alama 14 (asilimia 8.4). Wanafunzi waliopata alama 14 walikuwa kwenye kiwango kizuri sana cha ufaulu kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha, kwani walijibu kwa usahihi

vipengele vyote saba vya swali hili. Wanafunzi waliopata alama kati ya 10 hadi 12 walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kujibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6, kati ya vipengele 7.

Aidha, wanafunzi waliopata alama kati ya 6 hadi 8 walikuwa kwenye kiwango cha wastani cha ufaulu; hawa walijibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya vipengele saba. Wanafunzi waliopata alama kati ya 0 hadi 4, walikuwa kwenye kiwango hafifu cha ufaulu, ikimaanisha kuwa walishindwa kujibu kipengele chochote au waliweza kujibu kwa usahihi vipengele visivyozidi viwili kati ya vipengele saba.

Katika kipengele cha (i), wanafunzi waliweza kubaini kuwa Masatu ni Msukuma. Jibu hili ni kiashiria kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha kusoma habari (Majadiliano) kati ya Dihenga na Masatu na kubaini ujumbe mahsusi uliokuwemo katika habari hiyo.

Kipengele cha (ii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini mtindo anaopenda Dihenga kutumia katika kusalimia watu. Wanafunzi waliobaini kuwa Dihenga hupendelea kusalimiana kwa mtindo wa kukumbatiana, walikuwa na uelewa mzuri juu ya matakwa ya swali; hivyo, walijibu kipengele hiki kwa ufasaha. Pia, kwa kuwa swali hili lilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maisha yao ya kila siku, baadhi ya wanafunzi walihawilisha maarifa namna watu wanavyosalimiana katika jamii yao; hivyo, walijibu kwa ufasaha.

Katika kipengele cha (iii), wanafunzi walitakiwa kubaini jina la ngoma inayochezwa na watu kutoka kabila la Wazaramo. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika kipengele hiki kilikuwa kizuri sana kwani wanafunzi wengi waliweza kuandika *Mdundiko*. Jibu hili linaashiria kuwa wanafunzi walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kuelewa habari ipasavyo.

Katika kipengele cha (iv), wanafunzi walitakiwa kubaini jina (kutoka kwenye majadiliano) la kabila ambalo watu wake husalimiana kwa kushikana mikono. Wanafunzi walioweza kubaini kuwa ni kabila la Wasukuma, ambalo watu husalimiana kwa kushikana mikono, walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kujibu maswali yatokanayo na kifungu cha habari.

Kipengele cha (v) kiliwataka wanafunzi kubaini faida mojawapo (kutoka kwenye kifungu cha habari) ya kucheza ngoma ya mdundiko. Kiwango cha ufaulu katika kipengele hiki kilikuwa kizuri kwani wanafunzi wengi waliweza kubaini kuwa faida mojawapo itokanayo na kucheza ngoma ya mdundiko, ni *kuweka mwili imara*. Jibu hili lilihusiana na uzoefu wa kawaida wa wanafunzi kwani wanafunzi walielewa kuwa, licha ya burudani, ngoma hutumika kama chanzo kimojawapo cha mazoezi cha kuufanya mwili uwe imara.

Kipengele cha (vi) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini jinsi mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalivyoanza. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulibaini kuwa wanafunzi wengi walikuwa na uelewa jinsi mazungumzo kati ya Dihenga na Masatu yalivyoanza. Wanafunzi hawa waliandika kuwa

mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianza *kwa salamu au kwa kusalimiana.* Wanafunzi hawa waliweza kujibu kwa usahihi swali hili kwani walihusianisha ufahamu wao katika maisha ya kila siku kuwa watoto (watu) wenye tabia njema husalimiana au husalimia watu wazima wanaokutana nao (hata kama hawawafahamu) kabla ya maongezi mengine.

Kipengele cha (vii) kilipima uwezo wa wanafunzi kubaini jambo walilojifunza kutokana na majadiliano kati ya Dihenga na Masatu. Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika kipengele hiki kilikuwa kizuri kwani wanafunzi waliweza kueleza walijifunza kuwa ni *umuhimu wa kucheza ngoma na namna ya kusalimiana au kudumisha utamaduni katika jamii.* **Kielelezo Na. 1.7** kinaonesha mfano wa majibu mazuri ya swali la 3 kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo.

**Maswali**

(i) Masatu ni kabila gani? msukuma

(ii) Dihenga hupendelea kusalimiaje? Kwa kukumbatiana

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo. mdundiko

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono? Kabila la wasukuma

(v) Taja faida moja ya kucheza ngoma ya 'mdundiko'.

mwili unakuwa imara

(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje?

kwa kusalimiana

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo? Kusalimiana kwa kushikana mikono na kwa kukumbatiana na kucheza ngoma za mdundiko

**Kielelezo Na. 1.7** *kinaonesha sampuli wa majibu sahihi ya swali la 3 kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo.*

Kwa nyongeza, uchambuzi ulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kati ya 6 hadi 8, ikiwa ni sawa na kujibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 4 kati ya vipengele 7. Kufaulu huku kwa wastani kulisababishwa na ukosefu wa umakini au ujuzi wa kutosha katika kusoma habari kwa kina. Jambo hili lilisababisha waweze kujibu kwa usahihi vipengele vichache tu. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walijibu vizuri kipengele cha (i), (ii), na (iii) na kukosa vipengele vilivyobaki. **Kielelezo Na. 1.8** kinaonesha mfano wa majibu kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo aliyepata ufaulu wa wastani

**Maswali**

(i) Masatu ni kabila gani? MSukuma

(ii) Dihenga hupendelea kusalimiaje? kuku mbatiana

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo. Mdundiko

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono? ____

(v) Taja faida moja ya kucheza ngoma ya 'mdundiko'.

kupata fedha

(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje?

Yali anza kwa kutumia lugha

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo? ni mojifunza lugha

**Kielelezo 1.8** *kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata ufaulu wa wastani kwa kushindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (iv) na (vii)*.

Pia, uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walipata alama kati ya 0 hadi 4. Hii inaashiria kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali katika vipengele vingi. Hivyo, walijibu kwa usahihi vipengele viwili au kimoja au walishindwa kujibu kipengele chochote cha swali la 3. Kwa mfano, katika kipengele cha (i), wanafunzi wengi waliandika *Zaramo, Msafwa* au *Mnyaturu*. Majibu haya yalisababishwa na ukosefu wa maarifa ya kutosha juu ya majadiliano kati ya Dihenga na Masatu.

Katika kipengele cha (ii), wanafunzi wengi waliokosa swali hili waliandika majibu yasio sahihi, kama vile *hujambo*, *sijambo*, *kushikana mikono* na *shikamoo.* Hii inamaanisha kuwa

wanafunzi hawa hawakuelewa kifungu hicho cha habari, hali iliyosababisha wanakili baadhi ya maneno kutoka katika kifungu cha habari na kuyawasilisha kama majibu katika swali hili.


Katika kipengele cha (iii), wanafunzi wengi walijibu kwa kuandika ama *ngoma za sherehe*, *mdumange* au *sindimba.* Majibu haya ni kiashiria kuwa wanafunzi walijibu kulingana na ufahamu walionao juu ya ngoma za baadhi ya makabila Tanzania na siyo kutokana na habari waliyoisoma.

Kipengele cha (iv) kililenga kubaini ufahamu wa mwanafunzi juu (kwa mujibu wa majadiliano) ya jina la kabila linalosalimiana kwa kushikana mikono. Wanafunzi wengi waliojibu swali hili waliandika *Wasukuma* kama jibu sahihi. Huu ni ushahidi kuwa wanafunzi wengi walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya habari waliyosoma, au walijibu kwa kutumia ufahamu au uzoefu wa jumla walionao kuhusu jinsi watu wanavyosalimiana.

Wanafunzi wengi waliojibu kipengele cha (v) waliandika *kushirikiana* au *kuburudika*, majibu ambayo sio sahihi kulingana na muktadha wa swali, japo ni kweli ngoma huburudisha na husaidia kujenga umoja na ushirikiano miongoni mwa jamii husika. Huu ni ushahidi kuwa wanafunzi wengi waliopata kiwango hafifu cha ufaulu hawakuelewa matakwa ya swali. Badala yake, walijibu kwa kutumia ufahamu au uzoefu wa jumla walionao kuhusu faida ya kucheza ngoma za asili.

Katika kipengele cha (vi), wanafunzi wengi walikosa kwa sababu waliandika *hujambo* au *sijambo*. Hii inamaanisha kuwa, wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali. Hali hii ilisababisha wanakili baadhi ya maneno kutoka katika kifungu cha habari. Majibu haya kimsingi yanaelekeana na uhalisia, japo sio sahihi kulingana na muktadha wa habari, kwani jibu sahihi ni *kwa kusalimiana.*

Kipengele cha (vii) kilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu na wanafunzi wengi walipata alama nzima (2) kwa kuweza kuandika kwa usahihi funzo walilolipata kutokana na kifungu cha habari waliyoisoma. Baadhi ya majibu waliyoeleza wanafunzi katika kategoria hii ni pamoja na *umuhimu wa kucheza ngoma* au *kudumisha utamaduni* na *kuongeza ufahamu wa jinsi watu kutoka makabila mbalimbali* walivyo na namna tofauti za kusalimiana. **Kielelezo Na. 1.9** kinaonesha sampuli ya majibu hafifu ya wanafunzi katika swali la 3.


**Maswali**

(i) Masatu ni kabila gani? mimi napenda kusalimiana kwa kukumbatia

(ii) Dihenga hupendelea kusalimiaje? Ndiye mara nyingi ninasalimia watu mbalimbali

(iii) Taja aina ya ngoma wanayocheza Wazaramo. Ahsante

(iv) Kwa mujibu wa majadiliano hayo, ni kabila gani husalimiana kwa kushikana mikono? Tumasalimiana kwa kushikana mikono wewe

(v) Taja faida moja ya kucheza ngoma ya 'mdundiko'.

Na mimi pia napenda mdundiko kwa sababu mwili unakuwa imara

(vi) Mazungumzo kati ya Masatu na Dihenga yalianzaje?

hupendelea ngoma gani.

(vii) Umejifunza nini kutokana na majadiliano hayo? ooh! Hongera


Dihenga

masatu

***Kielelezo Na. 1.9** kinaonesha mfano wa majibu hafifu katika swali la 3*


### 2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu 3: *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* na umahiri mahususi wa *3.1: Kutumia ramani katika mazingira mbalimbali.* Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kusoma na kubaini alama mbalimbali za ramani zilizopo kwenye kipengele cha (i) hadi (iv) (Tazama kielelezo Na. 4.1) na kisha kuandika katika nafasi zilizo wazi alama hizo zinawakilisha nini katika ramani. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne: (i), (ii), (iii) na (iv). Kipengele cha (i) kilipima umahiri wa wanafunzi kubaini alama inayowakilisha daraja. Kipengele cha (ii) kilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini uelekeo wa *Kaskazini*. Kipengele cha (iii) kilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini alama inayowakilisha mto, na kipengele cha (iv) kilipima umahiri wa wanafunzi katika kubaini alama inayowakilisha reli. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 8. **Kielelezo Na. 1.10** kinaonesha alama mbalimbali za ramani zilizotumika katika swali la 4.




**Kielelezo Na. 1.10:** *Alama za ramani zilizotumika katika swali la 4*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,385 (100%). Kati yao wanafunzi 358,297 (21.04%) walipata alama zote 8 ambao ni ufaulu mzuri sana; wanafunzi 420,818 (24.72%) walipata alama 6, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine, wanafunzi 350,687 (20.60%) walipata alama 4, ambao ni ufaulu wa wastani, na wanafunzi 572,583 (33.63%) walipata alama 0 hadi 2, ambao ni ufaulu hafifu. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa ni cha wastani kwani wanafunzi 1,129,802 (66.37%) walipata kati ya alama 4 hadi 8. **Chati Na. 4** inaonesha kiwango cha ufaulu katika swali la 4.





***Chati Na.4:*** *Kiwango kizuri cha ufaulu wa asilimia 66.37 ya wanafunzi walioweza kupata alama 4 hadi 8*

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu katika swali hili ulibaini kuwa wanafunzi waliopata alama 8 walijibu kwa usahihi vipengele vyote vinne vya swali hili. Wanafunzi waliopata alama 6 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 kati ya vipengele 4. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliopata alama 4 walijibu kwa usahihi vipengele 2 kati ya vinne, na wanafunzi waliopata alama 0 hadi 2 ama hawakujibu kwa

usahihi kipengele chochote (walipata sifuri) au walijibu kwa usahihi kipengele kimoja kati ya vipengele vinne vilivyotolewa.

Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi katika kusoma na kutafsiri alama za ramani. Wanafunzi waliopata alama 8 walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma na kutafsiri alama za ramani.

Katika kipengele cha kwanza (i), wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha waliandika jibu sahihi *daraja*. Katika kipengele cha (ii), wanafunzi waliokijibu kwa usahihi walitambua kuwa alama hiyo iliwakilisha upande wa *Kaskazini* au *dira*. Katika kipengele cha (iii), wanafunzi waliojibu kwa usahihi walibaini alama iliyopo inawakilisha *mto* katika ramani na katika kipengele cha mwisho (iv), wanafunzi waliweza kubaini kuwa alama hiyo inawakilisha *reli*. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilidhihirisha umahiri wao kuhusu tafsiri ya alama za ramani. **Kielelezo Na. 1.11** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 4.


4. Je, alama zifuatazo zinawakilisha nini katika ramani?

(i) Daraja.


(ii) Dira.

(iii) Mto.

(iv) Reli.

**Kielelezo Na. 1.11** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vinne vya swali la 4*


Wanafunzi wengi waliopata alama 6 walikosa katika kipengele cha (ii). Wengi wao waliandika *mkuki, kanisa, mshale* na *mwelekeo wa juu.* Majibu yasiyosahihi katika kipengele hiki yanafanana sana na picha za baadhi ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yao. Kwa ujumla, kutokana na majibu yasiyosahihi inaweza kuhitimishwa kuwa wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha kati ya picha ya vitu na ramani ya vitu. **Kielelezo Na. 1.12** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi kipengele (ii) cha swali la 4.




**Kielelezo Na. 1.12:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (ii) cha swali la 4*

Pamoja na hayo, wanafunzi 350,687 (20.60%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele viwili kati vinne, hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Wanafunzi hawa walikuwa na uwezo wa wastani wa kusoma na kutafsiri ramani. Wengi wao

walishindwa kujibu kwa usahihi kipengele (iii) na (iv). Katika kipengele (iii), wanafunzi wengi waliandika *radi, kamba, miti, misitu, waya, umeme na mmea*. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawa walichanganya vitu wanavyoviona katika maisha yao ya kila siku kwani vitu hivyo vinauhusiano na alama iliyopo kwenye kipengele hiki. Katika kipengele (iv), wanafunzi walishindwa kutambua alama iliyowakilisha reli. Wengi wao waliandika *barabara, pundamilia, kamba, kuni, antenna, radio, waya* na *kijiti*. Vitu hivi vinauhusiano wa karibu na alama iliyopo katika kipengele hiki. **Kielelezo Na. 1.13** kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi kipengele (iii) na (iv) cha swali la 4.


4. Je, alama zifuatazo zinawakilisha nini katika ramani?

(i) DARAJA.


(ii) PANDE KUU ZA DIRA

(iii) UMEME.

(iv) PUNDAMILIA.

**Kielelezo Na. 1.13:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele cha (iii) na (iv) cha swali la 4*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi kipengele hata kimoja au walijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu. Hivyo, wanafunzi hao (572,583, sawa na 33.63%) walipata alama kati ya 0 hadi 2. Hali hii inayoonesha uwezo mdogo kabisa wa wanafunzi katika kutafsiri alama za ramani. Kati yao, wanafunzi 269,678 (15.84%) walijibu kipengele kimoja kwa usahihi kati ya vipengele vinne, na 302,905 (17.79%) waliandika majibu yasiyosahihi katika vipengele vyote. Kipengele cha (i) kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi katika kundi hili kwani waliweza kutambua alama hiyo kuwa ni *daraja*. **Kielelezo Na. 1.14** kinaonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mwanafunzi mmojawapo.


4. Je, alama zifuatazo zinawakilisha nini katika ramani?

(i) Ramani

(ii) maShaliki

(iii) Ramani

(iv) Ra mani

**Kielelezo Na. 1.14:** *Sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kipengele chochote katika swali la 4.*

## 3.0 TATHMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI

Uchambuzi katika Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2020 unaonesha kuwa, kati ya mahiri kuu nne zilizopimwa kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016, kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri katika mahiri mbili na cha wastani katika mahiri zingine mbili. Kiwango cha ufaulu katika umahiri wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* ni kizuri; ufaulu ulikuwa asilimia 68.40. Pia, kiwango cha ufaulu katika umahiri wa *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* ni kizuri kwa asilimia 67.34. Kwa upande mwingine, ufaulu katika umahiri wa *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ni asilimia 66.41 katika umahiri wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku* ni asilimia 66.37. Ingawa wanafunzi wengi walifikia umahiri unaokubalika katika mahiri zote nne kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari, wanafunzi hawa wana upungufu wa umahiri unaotarajiwa. Wana umahiri kidogo katika *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Shughuli za Kila Siku*. Kwa ufupi, juhudi na maarifa zaidi yanatakiwa katika kuwasaidia wanafunzi kupata umahiri unaokubalika katika mahiri zote nne.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha kiwango cha ufaulu cha mahiri mbili ambazo ni Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka na Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali kilikuwa kizuri. Aidha, mahiri nyingine mbili ambazo ni Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii na Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku zilikuwa na kiwango cha wastani

cha ufaulu. Kuna changamoto zilizosababisha wanafunzi wachache kutofanya vizuri katika umahiri uliotahiniwa. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa mahitaji ya maswali na kukosa au kuwa na maarifa kidogo. Wanafunzi wachache walionesha ujuzi hafifu katika kusoma na kuandika jambo lililosababisha washindwe kusoma au kuelewa matakwa ya maswali na kujibu kwa usahihi. Hata hivyo, wanafunzi wengine wameweza kuonesha umahiri wa kutosha uliyowawezesha kubaini majibu sahihi katika maswali yaliyoulizwa na hivyo kuwa na utendaji (ufaulu) mzuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi katika kuonesha matendo ya kusalimiana ya makabila mbalimbali ya Kitanzania na kutamka salamu hizo kwa ufasaha.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi katika kucheza na kuimba nyimbo za utamaduni kwa kutumia vifaa vya utamaduni.

(c) Walimu wawaongoze wanafunzi katika kuchora ramani na kuonesha alama za ramani na kuchora pande kuu za dunia.

(d) Walimu wapime umahiri wa wanafunzi katika stadi za kusoma na kuandika ili kuwasaidia wanafunzi walio na ujuzi mdogo wa kusoma na kuandika.

(e) Mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zitumike katika masomo yanayolenga kukuza ujuzi na ufahamu wa wanafunzi.

(f) Walimu wasisitizwe kufanya ziara za kimasomo katika maeneo mbalimbali yanayoweza kuwajengea wanafunzi kupata umahiri mahususi.

(g) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha yanayolenga kukuza umahiri ili kuwajengea uwezo katika kujibu maswali yanayopima umahiri.

**KIAMBATISHO**

**03 Maarifa ya Jamii - Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2019 na 2020**

| | Umahiri | UPIMAJI 2019 | | | | UPIMAJI 2020 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu wa kila swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu wa kila swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | % wa ufaulu | | | Namba ya swali | % wa ufaulu | | |
| 1 | Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka | 3 | 58.90 | 58.90 | Wastani | 2 | 67.34 | 67.34 | Mzuri |
| 2 | Kutambua Misingi ya Uzalaendo katika Jamii | 1 | 92.70 | 92.70 | Mzuri | 3 | 66.41 | 66.41 | Wastani |
| 3 | Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku | 4 | 59.50 | 59.50 | Wastani | 4 | 66.37 | 66.37 | Wastani |
| 4 | Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali | 2 | 47.60 | 47.60 | Wastani | 1 | 68.40 | 68.40 | Mzuri |